BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuwasilisha Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutujaalia amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zake zote ambazo ni muhimu sana katika maisha ya mwanaadamu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Baraza hili Tukufu kwa lengo kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wake wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa ushirikiano wao mkubwa kwa kamati wakati Kamati ilipokuwa ikijadili mswada huu kwa muda wa siku mbili na kufikia makubaliano ya pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** mswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na

mapendekezo mazuri ya Waheshimiwa Wajumbe, wadau mbali mbali kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti waliweza kutoa michango yao. Ni wazi kuwa, marekebisho haya yanalenga kuimarisha utendaji kazi

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inawashukuru na kuwapongeza wadau wote kwa kukubali kujumuika nasi kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujenga uelewa, maarifa na kuendeleza uhusiano katika utendaji kazi wa masuala mbali mbali ya kisheria. Miongoni mwa wadau hawa ni Prof. Chris Maina Peter Mwenyekiti wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Ndg. Masoud Rukazibwa kutoka Jumuiya ya ZLS, Ndg. Khamis Ngwali kutoka Jumuiya ya ANGOZA, Ndg. Ussi Makame Kombo kutoka CGCLA, Ndg. Chausiku Kuya kutoka Mahakama Kuu na Ndg. Shamsi Y. Saad kutoka Ofisi ya DPP Zanzibar.

Aidha, kamati yangu inawashukuru na kuwapongeza kwa juhudi zao na ufafanuzi wao walioutoa katika kujenga mazingira bora ya utekelezaji wa sheria hizi ambazo zinaenda kuweka taswira mpya ya utendaji wa taasisi za Serikali. Kwa Muktadha huo, kamati inawaomba kuendelea kuona umuhimu wa kusaidia kuunga mkono juhudi za Serikali kwa miswada inayokuja Barazani.

**Mheshimiwa Spika**, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa mswada huu. Kiukweli wajumbe hawa walizingatia misingi ya sheria na utawala bora na kusimamia malengo chanya na Azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa heshima naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| *4.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Abdallah Abass Wadi | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Panya Ali Abdallah | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, sambamba na wajumbe hao, kamati inambua na kuthamini msaada mkubwa kutoka kwa wasaidizi wake. Naomba pia kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 2. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 3. | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu na |
| 4. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha |

**Mheshimiwa Spika,** sina budi kueleza kuwa, mswada huu una lengo la kufanyia marekebisho baadhi ya sheria sita tofauti na vifungu tofauti, ambapo Serikali imeona ipo haja ya kufanya hivyo. Pia, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yanaonekana katika Marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa kwa ajili ya ufafanuzi na ufahamu zaidi wa vifungu vilivyopendekezwa kufanyiwa marekebisho na kamati kwa kuzingatia muktadha wa sarufi ya lugha na muundo wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza marekebisho ya Sheria mbali mbali, ambapo mapendekezo haya lengo lake ni kuondoa changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizi. Hivyo, katika utekelezaji wa Sheria hizi ni wazi kuwa zinahitaji kufanyiwa

marekebisho ili kuondoa changamoto zinazojitokeza katika Taasisi za Serikali katika maeneo mbali mbali ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia sehemu ya pili ya mswada huu ambayo imeainisha marekebisho ya Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam. 6 ya 2013 ambapo Serikali kupitia marekebisho haya inaenda kuiunganisha Tume ya Kurekebisha Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na hivyo Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria inafutwa na majukumu yake kutekelezwa kupitia sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia pendekezo la Mabadiliko ya Tume ya Kurekebisha Sheria kuungana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati imeelezwa kuwa Serikali ilifanya utafiti wa kutosha na hatimae kuja na mtazamo mpya wa kuondoa muingiliano wa kazi kwa taasisi hizi ikiwa na lengo la kuleta ufanisi wa kutekeleza majukumu yake, kuongeza nguvu ya utendaji kazi pamoja na kupunguza gharama za fedha kwa ajili ya uendeshaji wa taasisi hizi ilihali majukumu yao yanafanana kwa asilimia kubwa.

Aidha, kamati inatoa rai kwa Serikali kuendelea kufanya tafiti kwa sheria mbali mbali ambazo zitatoa miongozo kwa taasisi za umma ikiwa ni pamoja na kuboresha suala zima la utoaji wa huduma. Hata hivyo, natoa pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuratibu na kusimamia sheria ambapo kimsingi inasaidia sana utekelezaji wa utawala bora katika taasisi za umma.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaunga mkono mapendekezo ya mswada huu isipokuwa wasiwasi wa kamati hii ni kuachwa majukumu ambayo yalitekelezwa na Tume hapo awali na badala yake mkazo zaidi ukawekwa katika kukamilisha malengo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo yamefafanuliwa kwa wazi kupitia sheria yake. Aidha, mswada huu haukufafanua au kuweka wazi lengo la kuziunganisha taasisi hizi mbili

ambazo zimekuwa zikifanya kazi kwa muda mrefu sasa na athari zake zinaonekana katika sekta ya sheria.

Kwa mantiki hiyo, kamati inashauri kwamba ufafanuzi wa kina utolewe ili Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wapate ufahamu wa suala hili. Aidha, kamati inashauri kuundwa kwa kurugenzi ambayo itafanya kazi zote zilizokuwa zikifanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo itakua chini ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka sawa maudhui yaliyokusudiwa na muundo uliotumika kwa mswada huu, kamati inashauri katika ***kifungu cha 13*** cha mswada huu kurekebishwa kama ifuatavyo:

i. Kwa kuingizwa maneno **"katika kifungu kidogo cha 1"** baina ya maneno **"kinarekebishwa**" na **"kwa"**.

ii. Kwa kuingizwa neno **"kidogo"** mwishoni mwa kifungu hicho.

**Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kwamba nchi yetu ipo katika mapambano makubwa ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kwa kuweka sheria kali na miongozo ambayo itasaidia kupunguza au kuondosha kabisa matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya ambazo zinaathiri kwa kiasi kikubwa nguvu kazi ya Taifa letu. Hivyo, ni wazi kwamba Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Nam. 8 ya 2021 ni lazima kufanyiwa marekebisho ili kuwa na utekelezaji mzuri katika kuendesha mashauri ya kesi na kuwatia hatiani wahalifu ambao hutumia kipengele cha mapungufu ya sheria hii kuendesha harakati zao za kihalifu.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli usiopingika kuwa hakuna sekta yoyote iliyoendelea bila ya kuratibiwa na kusimamiwa ipasavyo katika utekelezaji wa majukumu yake, hivyo ni vyema tukazingatia miongozo mbali mbali inayotolewa na juu ya taasisi hizo. Kwa msingi huo, kamati imekuwa ikifanya ziara za mara kwa mara katika taasisi hii na kupata malalamiko ambayo

mashauri yanayohusu Dawa za Kulevya yanashindwa kuendelea Mahakamani kutokana na mapungufu yaliyomo katika sheria yao. Kwa mnasaba huu, kamati imeridhika na marekebisho yatakayofanywa katika ***kifungu cha 42*** cha Sheria Mama baada ya kuondoa mwanya unaotumika kuwaachia huru wahalifu wa Dawa za Kulevya kwa kipengele cha shahidi huru.

Aidha, kamati imeridhia marekebisho ya ***kifungu cha 20*** cha mswada huu chenye marekebisho ya ***kifungu cha 46*** cha Sheria Mama ambacho kinaweka masharti bora zaidi katika utekelezaji wa kifungu hiki kwa kuzingatia misingi ya haki na sheria ambayo imelindwa vyema katika Katiba yetu ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeridhia marekebisho ya Sheria ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar, Nam. 4 ya 2003 katika **kifungu cha 3** cha Sheria Mama ambapo hapo awali maana ya kifungu hiki haikuwa wazi. Hata hivyo, katika sehemu hii kamati inashauri kufanywa marekebisho ya ***kifungu cha 28*** cha mswada huu kwa kurekebishwa kama ifuatavyo: -

a) kufutwa neno **"maneno"** liliopo baina ya maneno "**wa"** na **"Miundombinu"** na kuwekwa badala yake neno **"neno".**

b) kufutwa maneno **"neno "Taifa" kabla ya neno "taarifa"** na kuwekwa badala yake maneno **"maneno "Taifa cha" kabla ya neno "kuhifadhia".**

**Mheshimiwa Spika,** kamati imefarijika sana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuridhia na kuviwezesha vikosi vya KMKM na KVZ kufanyiwa marekebisho katika sheria zake, ambapo sasa vikosi hivi vinaenda kufanya shughuli za uzalishaji mali na kukuwa kiuchumi, kibiashara na uwekezaji ili kwenda sambamba na kazi zake kwa mujibu wa sheria. Hatua hii ni kubwa na ni ya kuungwa mkono kwani vikosi vyetu vinaenda kuimarika katika shughuli zake za uendeshaji na kujipambanua katika ushiriki wake wa maendeleo ya nchi yetu.

Sambamba na hayo, kamati yangu inaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kutoa sehemu ya fedha zitakazopatikana kwenye vikosi hivyo katika kazi zao za kibishara kupatiwa angalau kwa asilimia thelathini ili zitumike kwa kuimarisha shughuli za vikosi vyao na kupunguza utegemezi wa fedha za ruzuku kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe hotuba hii kwa kuishauri Serikali wakati wa kufanya marekebisho ya miundo ya taasisi kwa kuziunganisha pamoja na kuhakikisha kuwa utafiti wa kina umefanyika kwa kuangalia athari za sasa na baadae ili kuepusha baada ya muda mfupi sheria na miundo ya taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** namalizia kwa kusema kuwa utekelezaji wa sheria unahitaji jitihada na utashi wa pamoja baina ya viongozi, watendaji, wananchi na wadau mbali mbali. Ikumbukwe, Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kimkakati ili kuhakikisha sheria zinazotungwa zinakuwa na tija katika kuwahudumia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya kamati yangu, naomba Kuwasilisha.

..................................

**(Mhe. Machano Othman Said)**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.**

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR